REPUBLIC OF KENYA

COUNTY ASSEMBLY OF LAIKIPIA

THE HANSARD

Tuesday, 21st May, 2024

The House met at the Assembly Chambers at 10.00 a.m.

[The Speaker (Hon. Lantano Nabaala) in the Chair]

PRAYERS

QUORUM CALL

Speaker: Thank you. Clerk, confirm if we have quorum.

(Lack of quorum confirmed)

Speaker: I direct that the bell be rang for ten minutes.

(Quorum bell rang for one minute)

Hon. Salim Edung: Hon. Speaker, we now have the quorum.

Speaker: Clerk confirm if that is the case.

(Clerk confirmed achievement of Quorum)

Speaker: Thank you. Now that we have quorum, let us proceed with the business of the day. The bell should now stop ringing.

MOTION

PROVISION OF FLOOD VICTIMS IN THE COUNTY WITH BASIC NECESSITIES

Hon. Catherine Umija: Thank you, Mr. Speaker. I beg to move the following motion;

THAT AWARE THAT pursuant to Article 43 (1c) of the Constitution of Kenya 2010, every person has the right to be free from hunger and to have adequate food of acceptable quality;

FURTHER AWARE THAT the Laikipia County Disaster Risk Management Act, 2019 defines disaster as progressive or a sudden, widespread or localized, natural or human-caused occurrence affecting the functioning of an entire or a section of community which;

a) causes or threatens to cause- death, injury or disease; damage to property, infrastructure or the environment; or disruption of the life of a community; and

b) is of magnitude that exceeds the ability of the community affected by the disaster to cope with its effects using only its own resources;

CONSCIOUS OF THE FACT THAT the Country has been experiencing heavy downpour rainfall which has caused floods in various parts of the country, leading to destruction of properties and loss of lives;

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor*

CONCERNED by the huge damage of farm crops and displacement of people by floods in Laikipia County; Alarmed by the status of the camping sites where the displaced persons have inadequate food stuffs, blankets and shelter;

APPRECIATING THAT section 10(2) of the Contingencies Fund and County Emergency Fund Act, 2011 stipulates that, the purpose of the emergency fund is to enable payments to be made in respect of a County when an urgent and unforeseen need for expenditure arises for which there is no specific legislative authority;

This House URGES the County Government to assist the flood victims with food, blankets and shelter.

Mr. Speaker, I just want to urge the County Government. We have realized that despite the heavy down pour of rainfall and we are seeing that there is small amount of rainfall right now. I know that we have people who have been displaced by the floods in Laikipia County and they are residing in camping sites. The persons have inadequate food, blankets and shelter.

As a County Government, I know we have the Disaster Risk Management Department that deals with it. We are asking the County Government to release the funds for disaster management so that they will be able to manage the people that are living in the camp sites who are having inadequate food stuff, blankets and shelter.

We know it is a right of every Kenyan and every person in the county to get food, shelter and clothing. This is part of the basic needs. This morning, we want to ensure that the County Government is doing its end of bargain to ensure that our people have adequate food, shelter and clothing. Thank you, Mr. Speaker. I would like to call upon the Deputy Speaker to second this motion.

(Hon. Anthony Theuri seconded)

(Question proposed)

Speaker: Hon. Members, I want to allow Hon. Stephen Ndiritu to take the floor.

Hon. Stephen Ndiritu: Asante, Mheshimiwa Spika. Nasimama kuunga mkono huu mswada mkono ambao umeletwa na Mheshimiwa Umija. Huu ni mswada ambao umeletwa kwa wakati ambao unafaa. Serikali iko na jukumu la kulinda mwananchi na kuhakikisha kuwa wananchi ambao wameadhirika wameweza kushughulikiwa kwa njia ambayo inafaa. Jambo lingine ni kwamba mswada umekuja kwa njia ambayo inafaa kwa sababu ni wakati huu tu ambao tunazungumza hapa. Watu wameweza kuadhirika.

Bwana Spika, ni juzi tu tumeona biashara katika Nanyuki na familia kadhaa katika Kijiji cha Likii zikisombwa na maji na wananchi kutoka Ruai, Kilimo na kwingineko katika Wadi ambayo ninawakilisha wakihangaishwa na mafuriko. Bwana Spika, wakati wowote tunafanya bajeti huwa tunatenga pesa za dharura. Mafuriko ni moja ya jambo dharura ambazo zinafaa kushughulikiwa haraka iwezekanavyo.

Bwana Spika, kuna pesa ambayo tulitenga kwa kiwango cha asilimia mbili kwa bajeti yote ya Kaunti na nchi nzima ili kuweza kushughulikia janga za dharura. Wananchi wanateseka na kuadhirika ilhali hatuoni serikali kwa njia yeyote ndogo ama kubwa ikiweza kuwashughulikia wale ambao wameadhiriwa. Juzi wakati kulikuwa na waadhiriwa katika Kijiji cha Likii niliona Serikali ikienda kupeleka sahani mbili, vijiko viwili na godoro nyembamba kama ngozi ya ng'ombe.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor*

Bwana Spika, hiyo ni kukosa kudhamini mwananchi wa hii Kaunti. Pesa ambazo tumetenga ni nyingi sana na zinafaa kuwashughulikia. Wanafaa kupewa mahali pazuri pa kulala, chakula na wanafaa kushughulikiwa kwa njia yeyote ambayo inawezekana kwa sababu tuko na hiyo pesa. Ni wakati mwafaka ambapo mswada umekuja hapa ili tuweze kujua serikali imetumia pesa za dharura kwa njia ipi.

Ni lazima tuelezwe kinagaubaga na waziri na afisa mkuu wahusika. Watueleze hizo pesa wametumia kwa njia gani hasa wakati huu wananchi wameadhirika. Barabara zimekatwa na maji. Si watu wamekuja na panga, si lori na tingatinga zimekuja kusukuma bali ni maji imesomba hizo barabara. Juzi tumesikia Doldol imefungwa siku nzima. Kwa siku nzima, lori na wananchi wamekaa. Hawajaweza kwenda kwa biashara zao kwa sababu ya laga kuteremka na kufunga barabara.

Serikali inafanya nini? Hiyo barabara si ya jana, ni ya tangu nizaliwe na tumekuwa tukitenga pesa ya Serikali Kuu na Serikali ya Kaunti. Tunataka kujua tutaishi hivi mpaka lini? Barabara ya Doldol itafunikwa na laaga mpaka lini? Tuko na pesa ambazo zinaweza kujenga daraja kubwa na mafuriko yakija, yanapita chini na wananchi wanasonga na kuendelea na shughuli zao. Tukikaa tukiangalia serikali na kuisifu kila wakati, tutaishi na shida.

Juzi niliona Mheshimiwa Boni Khalwale alipokuwa akizungumza Seneti na kuuliza, ni lini viongozi ambao wako upande wa serikali kama mimi na wale wengine ambao hawajaingia kwa hizi viti, watakaa na waambie serikali wanafanya vibaya. Hatukuchaguliwa kusifu serikali kila wakati. Kama ni kubaya tunasema ni kubaya. Kama pesa ya kufanya kazi haitolewi, tunasema haijatolewa.

Tukikaa hapa kila wakati tukisifu na kuweka urafiki, tutashughulikia mwananchi lini? Pia tunataka kuwasukuma wale ambao wako upande wa upinzani. Ni lazima wawe kipao mbele. Tunaposema haya mambo, ninafaa kuwa nikisikia upinzani wakianza. Ninashukuru kwa sababu jambo la kwanza ni wameleta mswada. Wameanza kufunguka na kuona ni lazima tuhakikishe ya kwamba wananchi wetu wanashughulikiwa.

Mimi nikiwa Mjeledi wa walio wengi Bungeni, niko upande wa serikali na ndio maana ninasema ni lazima tuelezwe hizi pesa zinafanya nini. Si kusema ninapinga serikali ama niko na nia mbaya na serikali. Ninataka kuona hiyo pesa inatumika kwa njia gani na wananchi wanasaidika aje. Kama pesa imetoka, imetoka ngapi? Ni akina nani wamepewa? Kama hazijapeanwa ziko na akina nani na anakusudia kufanya nini nayo?

Hayo ndio maswali ambayo tunafaa kuuliza kama Wabunge. Tukikaa hivi, pesa itachukuliwa, itatumika, watu wataenda mandari kujivinjari na pesa ya wananchi itatumika kwa njia ambayo haifai. Huu ndio wakati mwafaka. Kesho tutakuwa na Waziri wa Fedha. Siku hizi tukiwaita waziri, wanaona wakiwa wakubwa hata tukiwaita wanasema hao ni waziri. Hawa ni wanakamati wakuu. Kuwaita waziri hapa ndio imetuletea shida. Waziri yuko Serikali Kuu, kwa hivyo hapa ni wanakamati wakuu wa kamati wakiongozwa na Gavana.

Majina ambayo tunawapatia zinawapatia kichwa ngumu. CO anaitwa jina na kujiona yeye ni mkubwa na ukimpigia, simu hashiki. Juzi nimesikia Mama yao akilia hapa na kusema hawachukui. Hiyo ni kukosa aibu. Wanafaa kuheshimu miaka ya mama yao. Akikupigia simu, unafaa kuchukua. Mama yao yuko na huo umri akiwakilisha wananchi lakini akipiga simu haichukuliwi. Hapigi simu kuomba ila anapiga kwa sababu ana jambo ambalo anataka kushughulikia wananchi wake.

Hilo ndilo tunataka kufanya. Sisi Waheshimiwa ni lazima tuungane na tuwe kitu kimoja. Bwana Spika, kama hatutajiheshimu katika Bunge hili, basi hatutaheshimiwa. Kama

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor*

tunataka pesa katika idara na inakosa kutumika vizuri ilhali tukikutana na hao tunawasifu, tutaishi na shida. Bwana Spika, nimesimama kidete na kusema ni lazima tuelezwe. Waziri akikuja kesho, ningetaka kuwaalika Waheshimiwa wote hata wa upinzani katika huo mkutano ili tuulize maswali.

Kamati inafanya kazi kwa niaba ya Bunge. Nimeona sote tuwe hapo ili tuweze kuelezwa pesa ilienda wapi, iko na nani, ameweka benki gani na tutaiendea lini ili iweze kuwasaidia wananchi. Bwana Spika, kwa hayo machache ninataka barabara zitengenezwe. Wale ambao wameadhirika waweze kushughulikiwa na waweze kupatiwa huduma ambazo wanafaa kupatiwa kwa sababu tulitenga pesa na iko. Asante, Mheshimiwa Spika.

Hon. Anthony Theuri: Asante sana, Bwana Spika. Ninashukuru kwa hii nafasi. Mimi ni mmoja wa kuunga huu mjadala mkono. Sheria inasema kwamba unafaa kuongea mara moja kwa mjadala. Sikuwa nimejitayarisha vizuri na ndio maana niliafiki bila kuchangia. Haya maisha yanataka ujanja. Nashukuru Mheshimiwa Umija kwa sababu ya huu mjadala. Ninashukuru kwa sababu umetoka mahali ambapo panastahili kutoka.

Mheshimiwa Ndiritu alikuwa amejitayarisha kurusha makombora upande ule mwingine lakini upinzani unaonekana umesimama na umejitayarisha kabisa. Huu mswada umekuja kwa wakati ambao unafaa. Mimi ni muadhiriwa na bado sauti yangu haijarudi. Wiki moja ambayo imepita tumekuwa tukiadhiriwa na mafuriko. Bwana Spika, cha aibu ni kwamba sisi kama kaunti tuko na shida kubwa sana.

Tuko na Saratani na kama si ya mafikira, ni saratani ya tabia. Wakati Kaunti iliitwa, tulijibu watu kadhaa wa Kaunti. Aibu ni kwamba hatujijui. Hakuna mtu ambaye hajui mimi ni mwakilishi wa Wadi ya Nanyuki. Hakuna mtu hajui Gavana na naibu wa Gavana ni nani. Hakuna mtu hajui Kamati ya kikao cha Gavana ambacho huwa kinafikiria mambo ya Kaunti lakini tumefika mahali siasa imetuingia na tunanyongwa na nyama ambayo iko kwa sahani badala ya ile ambayo iko kwa mdomo.

Wakati tunafika hapo, laiti ungeniona Mheshimiwa Spika. Karibu nitoe suruali ambayo nilikuwa ninarudishwa na akina mama nikijaribu kuokoa maisha ya watu. Sio kujifanya kwa sababu ndugu zangu na familia yangu ilikuwa imeadhirika. Kaunti inapoenda hapo hawaendi kuokoa ila wanaenda na kamera mingi kuliko usaidizi. Wanaenda na propaganda na wakati tunaokoa maisha, wanasiasa wanapinga. Wanawaambia wakumbuke wanataka uongozi fulani. Hiyo ni aibu na sikuji hapa kudanganya.

Siku nyingine iliyofuata Mheshimiwa Ndiritu anaongea ukweli hata kama hakujua ya kwamba walikuja na blanketi, sahani mbili, vijiko viwili na ukweli ni kwamba mimi ni shahidi kwamba usaidizi mingi ilitoka kwa msalaba mwekundu. Wale wengine ambao walitoa usaidizi mkubwa ni Serikali Kuu ikiongozwa na DCC wetu. Sisi tulienda kusindikisha. Bwana Spika, naomba Mungu atuweke vizuri kesho na ninaomba Waheshimiwa wabebe maswali.

Mimi niko na rekodi ya kutoka nichaguliwe hadi sasa ya mikasa yote ambayo imetupata iwe ni ya moto, upepo ama maji na hiyo yote nitaweka hapa pamoja na usaidizi ambao umetoka. Kwa sababu Mheshimiwa Wachuka tuko na kijiji kikubwa sana cha Igwamiti, aje na yake. Mheshimiwa Kagondu wa Thingithu na Waheshimiwa wengine wote waje na tuangalie pesa ambayo imetumika ya mambo dharura kwa wananchi inatusaidia aje.

Bwana Spika, ninapoongea hapa, ieleweke kwamba Mwakilishi wa Wadi ni wa kuomba na ndio maana tunakosewa aibu. Unapigia CO ambaye sijui ni wa kampuni gani lakini mimi ndiye CO kwa sababu mimi ni Rais wa Wadi ya Nanyuki. Ukikuja kwangu Nanyuki, hata kama

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor*

wewe ni Spika, wewe ni Spika hapa lakini ukija Wadi ya Nanyuki mimi ndiye Rais. Ninakukaribisha kama Rais wa nchi nyingine kwa sababu hii ni nchi nyingine

Majina mengine hapa yanastahili kuondolewa kwa sababu mwakilishi wa wadi hana lake. Hata saa hii nikitaka kupelekewa maji shuleni itakuwa aibu. Wakati kumekuwa na mvua kubwa nilienda kwa Afisa Mkuu wa Wizara ya Maji na karibu mwezi umeisha. Nilimwambia kuna milioni yangu moja ambayo niliweka kwa bajeti na nikapatia kikundi fulani cha maji. Sasa karibu mwaka unaisha. Tumebakisha wiki tatu ili mwaka wa serikali uishe. Niliwaambia Watu wa Nkando hawana maji na kwamba wanakunywa maji ya mvua ama mto kwa sababu mifereji yao yote ilibebwa na maji.

Bwana Spika, hadi wa leo Afisa Mkuu hachukui simu, Waziri hachukui simu na mkurugenzi ananicheka kwa sababu walifika. Jambo kubwa ni aibu na ninaomba haya maombi yafikie Mwenyezi Mungu kwa sababu huwa anasikia maombi yangu na wateule kama nyinyi. Ile siku tutapata fedha za wadi ndio itakuwa dawa yetu. Bwana Spika, saa hii unasikia watu wangu hawana maji na ni wakati wa mvua. Ukienda huko, afisa mkuu anakuangalia na kukuchekesha. Yeye anasema ni mtoto wa Gavana na hakuna mahali utampeleka.

Mheshimiwa Spika, mimi nimeamua. Gavana ni rafiki yangu, tulimletea Spika na nitashikilia mahali nitaweza lakini ikifika ni kazi, sijafikisha miaka arobaini na sitarudi kuchomelea mahali nilikuwa. Sitaharibu maisha ya siasa kwa sababu Gavana ni rafiki yangu. Nikirudi, nitakuja na taarifa ya afya na kilimo. Kesho nitaleta ya Waziri wa Kilimo. Tumekuwa tukiaibika wakati Mjumbe yuko na milioni mia mbili na siwezi taja miradi mitatu. Ninakaa chini na kusema kuwa nimeleta salamu za Gavana na kwamba tutafanya maendeleo fulani.

Tumekuwa tukihubiri injili ya uongo na ya kungoja. Wakati Mjumbe amesimama anataja miradi yake bila kudanganya. Atasema ng'ombe ikienda asubuhi na irudi saa nane kukunywa maji, ikikamuliwa bado akiyataja miradi yake kwa sababu yuko na pesa. Sisi kwa sababu tulikubali kuolewa, tukakubali siasa ya ujinga, nilionyeshwa Mheshimiwa Umija ni mbaya, nilionyeshwa Mheshimiwa Moile ni Maasai, nilionyeshwa mama yao ni mama na nilionyeshwa Kawambui ametoka Ghetto hafikirii vizuri ndio tukakubali kugawanyishwa.

Saa hii, ni aibu na Laikipia ikitolewa, niko na uhakika tuko chini kwa maendeleo. Tulisahau kazi yetu ya uangalizi tukawa marafiki na wale watu wengine. Bwana Spika, nilikuwa ninasoma kitabu fulani na mama fulani akasema maneno mengi na jambo muhimu nilisikia ni kwamba kama unataka watoto wako wawe na adabu na wakuletee heshima katika maisha yako ya uzee, usiwe rafiki na watoto wako. Kuwa mzazi. Wakati utakuwa mzazi uwapatie nidhamu, basi watakuheshimu.

Hata sisi unapotuona hapa Bwana Spika, ni kama wazazi wa hao watu. Kama hatukuchaguliwa na kama hawa Waheshimiwa hawakuteuliwa na vyama vyao, kama Mheshimiwa Leshuel, Mheshimiwa Mary wa Chama cha UDA na Salim hakungekuwa na Mawaziri na Afisa Wakuu. Sisi ndio wazazi wao na tumesahau kazi yetu. Tumejifanya wazuri sana. Laiti tungekuwa tunaongea Kikuyu, ningekupatia msemo mmoja hungewahi kusahau lakini kwa sababu sisi ni watu wazima, sitasema hilo.

Mheshimiwa Spika, ninaomba Bunge hili kama tunataka kuheshimiwa nyumbani, kama tunataka kutoa magavana hapa na Rais na kama tunataka kutajirika kwa haki, ni lazima tuwajibike. Tuulize maswali kisha usalimie mtu na umwambie hatuna ubaya ila tunafanya kazi yetu. Mwananchi hana aibu na nilisema hapa. Nikimalizia, mimi nimejenga barabara ambazo hazijafika kilomita ishirini na niko mwaka wa pili. Niliambia wananchi nitawatengenezea kilomita zaidi ya mia tatu.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor*

Mheshimiwa Spika, mimi ni binadamu mimi si mchungaji na mimi si mganga kwamba nitafanya *abracadabra* barabara ziwe. Sitafanya *abracadabra* kuwe na lami. Ni lazima kazi ifanywe. Bwana Spika, saa hii nikisimama hapa na nikiwa Wadi ya Nanyuki, najua kila mtu hapa ni mwanahisa wa huu mji. Kuna idara moja ya maji ya NAWASCO ambayo inatupatia milioni 1.2 kwa kila mwezi. Tulienda na Gavana na kuwaambia watununuliwe chombo cha kuchimbua kisima.

Bwana Spika, hata kama ni wewe, wakati unapika unaanza wewe mwenyewe kwa kusikia kama chakula kina chumvi ili wageni pia waamini kwamba hiyo chakula haina simu. Bwana Spika, sasa ni mwaka unaisha na hakuna mtu ambaye anaweza kusimama hapa na kusema ni wapi kisima kimechimbuliwa. Hizo lori mbili za kuchimba visima zimenunuliwa na pesa ya watu wa Wadi ya Nanyuki. Hazijawahi kuchimbua hata shimo moja la choo ama kisima kimoja. Kisha unaniambia wanatubeba vizuri.

Ninaomba kwa heshima, hili Bunge letu lijijue na lifanye kazi vile inastahili. Hizi pesa ambazo tunafikia hata saa hii kuna watu ambao wanalala nje kwa sababu ya mafuriko. Chakula ambayo tuliwapatia kilo tano imeisha. Kuna watoto ambao hawajarudi shule. Mheshimiwa Spika, wakati tunaongea hapa wengine niliwapeleka hospitali ili washauriwe. Bwana Spika, ningeomba tuunge mkono huu mjadala.

Kamati ambayo inaongozwa na Mheshimiwa Leshuel ya Utekelezaji, wanafaa kufanya bidii ili tuone kazi yao nikiwa kiranja wake, nitamwangalia. Mijadala ambayo inapitishwa hapa iwe inafuatwa. Ninaomba tukitoka hapa Mheshimiwa Spika, utumie nguvu yako yote kwa sababu ninataka kuwa muungwana. Ninapigana katika Bunge hili na tukitoka huko, niwe rafiki ya kila mtu. Walienda huko na kukuta kuna watoto ambao wamelemaa na wazazi wao walikuwa wamewafungia kwa nyumba.

Walisema watawapeleka shule lakini hadi leo wakipigiwa simu, hasa Naibu wa Gavana hawezi chukua. Yeye mwenyewe ndiye alienda na sisi tunasema huwezi kuleta mzaha wa chakula kwa mtu aliye na njaa. Bwana Spika, nauliza utumie nguvu zako. Piga simu zote ili watu wa kwangu wasaidike. Saa hii, kuna shule yangu ambayo haijafunguliwa ambayo inaitwa Likii Special School ambayo inashughulikia watoto walemavu. Bwana Spika, hadi leo hawajafungua kwa sababu ua ilienda na maji.

Naibu wa Gavana alikuja na kusema ya kwamba serikali itafanya na wale Watoto wakapiga makofi. Ungelia machozi ukiona mwenye alidanganya na hadi siku ya leo, hapatikani kwa simu. Ninamtaja jina kwa sababu ni ukweli. Tutatoka hapo na kuteremka kwetu, tukasema hizo familia Hamsini, sisi kama serikali tutawatafutia nyumba na tulipie watoto wao shule na kuwanunulia sare za shule.

Mheshimiwa Spika, mimi naishi na hao watu na kila asubuhi, hao huja kwangu au kupiga simu wakiuliza. Mimi nikienda kuuliza wanajibu eti napiga Gavana. Kwani Gavana, amekuwa ni nguo chafu kila mtu awe akajipanguza naye? Watu waache kujificha nyuma ya Gavana na waje hapa. Tutawafuta kwa sababu yule mtu ambaye alikuwa anakalia kile kiti cha Wodi ya Nanyuki, nilisema ya kwamba nitafanya kazi nzuri kumshinda na raia huwa hawasamehei mtu.

Kama haufanyi kazi, watakutoa na mimi sitaki kutolewa kwa sababu ya makosa ya mtu. Nitasema na kama Mheshimiwa Spika hautanisikia hapa, niko na mdomo kubwa na kwa hivyo, nitazunguka huu mji nikisema ukweli. Nitasema makosa ni ya fulani, na niseme ni nani ambaye ameiba ili wananchi wachukue hatua mkononi.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor*

Kabla tufikie hapo Mheshimiwa Spika, simama nasi. Kwa hayo machache au mengi, naunga huu mjadala asilimia mia kwa sababu ni lazima watu wetu wasaidiwe. Hili Bunge kama lina usaidizi, waje wanisaidie pale mashinani na wapate kuona yale ambayo yanaendelea.

Hon. Irene Wachuka: Asante sana, Bwana Spika. Nimechelewa kidogo kwa sababu ya mambo machache kama vile Naibu wa Spika alivyosema. Unajua sisi huwa hatulali. Mapema kabla utoke, unapatana na hao watu na ni vizuri kwa sababu wanafanya kazi yao. Walitupatia nafasi ya kuhudumia wananchi. Nataka kushukuru Mheshimiwa Catherine Umija ambaye ameleta mjadala muhimu sana.

Wiki iliyopita, Naibu wa Spika alikuwa na niliongea kuhusu wale watu ambao waliokuwa na singetaka Naibu wa Spika leo atoke kabla sijaongea leo. Nilikuwa nasema kuhusu vile kazi inatendwa hapa na wale watu ambao wamepewa kazi na Gavana. Nikaongea kuhusu mipangilio ya janga ambayo imetokea Kenya nzima. Nimeshangaa kuhusu kijiji cha kwangu ambacho kinaitwa Kia-Maina. Kulikuwa na watu wengi sana ambao walikuwa na shida na nikawapelekea godoro kumi na nne kutoka kwa mshahara wangu.

Kulikuwa na harambee ya kuchangia hao watu na mwenye kusimamia *administration* anayeitwa Kendi Gitonga, akasimama na kutoa elfu tano. Mimi nikazindikisha godoro zangu na elfu tatu, Waziri wa Kilimo, Kasoo akatoa tano, Waziri wa Ujenzi na Barabara, Kibara akatoa tano na Waziri wa maji akatoa kumi. Kendi alisimama na kusema ya kwamba kesho yake ataleta blanketi na godoro zingine. Nataka Wajumbe wasikie ya kwamba alileta vitu Jumamosi na hata hakusema.

Huko sio kwake na amechaguliwa na Gavana lakini mimi nilipewa kura na wananchi wa Igwamiti na hayo ni mambo ambayo yanafaa yasikike.

Kabla sijakuja hapa, nimetoa taarifa hapo nje kwa ofisi yangu na ndio maana nimechelewa kidogo. Kendi alileta godoro na blanketi. Ukiangalia katika bajeti yetu ya pesa za janga za dharura, alisema ya kwamba zile vitu ni zake. Watu walianza kuuliza ni kwa nini niliwaahidi ya kwamba kuna pesa ambazo hushughulikia janga za dharura ilhali hao wanasikia ya kwamba Kaunti zingine zinaletewa vitu na lori kwa sababu hiyo ni mali ya umma.

Bwana Spika, ni hadi ile siku ambayo mtaleta mtu mmoja au wawili kama mnataka. Nikiongea hivyo, Mheshimiwa kutoka Marmanet anajua ya kwamba tulileta Tabitha Mbiriri aliyekuwa Waziri wa Elimu na Daktari Lenai aliyekuwa Waziri wa Afya wakakaa hapa. Kulikuwa kukali na wakati huo nilikuwa nimeteuliwa na niling'ang'ana na hao watu wawili na walitokea mlango ule. Ni mpaka tulete watu wawili na tusaidiane.

Wakati wa kushikana ni lazima tushikane. Sijui kama ushawahi kusikia punda inapojua ingine iko na shida, inaanza kutoa sauti ya *Hee hoo! Hee hoo*! na mwenzake anajibu *Hee hoo! Hee hoo*! Ni lazima tufanye hivyo na tulete watu wawili. Wa kwanza atoke Wadi ya Igwamiti anayeitwa Kenneth Kibara. Hauwezi ukaingia kwangu hadi nyumba za Kaunti ambazo mimi nilikuwa nimejenga hadi unakuja kupatia warembo na wale watu ambao unataka eti ni siasa.

Ninaeleza naibu wa Spika kupitia Bwana Spika, nikinyenyekea utuitie Gavana sisi zote kama Bunge ili watuambie ukweli wa mambo. Tuwache kuongea hapa ilhali hatumwambii. Aje tumwambie fulani na fulani watakanyanga kubwa kubwa ili watoke wakafanye siasa na tuletewe wafanyikazi ambao watafanyia Wanjiku kazi. Yeye hakuna mtu aliyempatia kura kwa sababu alipewa kiti na Gavana.

Mheshimiwa Kanyutu amepewa na watu wa Marmanet na mimi nimepewa na watu wa kwangu. Hawa Waheshimiwa wa kuteuliwa wameletwa hapa na chama ili kuangalia kazi yetu na tunafanya kazi pamoja. Ukiangalia vile Waheshimiwa wa kuteuliwa wanafanya kazi,

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor*

wanaonyeshana ya kwamba wako na moyo safi wakiwa chini ya serikali inayoongozwa na Raisi Ruto na Rigathi Gachagua.

Kama mnataka tufanye chochote katika hili Bunge, wacha tulete watu wawili hapa. Hapa hapatakuwa na mchezo na kama mtaogopa, mlete tuwaonyeshe. Hata wa leo Lenai na Mbiriri hawako katika hii serikali. Ukiangalia ile pesa ambayo tunaweka ikiwa nyingi kwa bajeti ni ya afya na maji kwa sababu kila mtu anaweza kuwa mgonjwa na pia kila mtu huhitaji maji.

Kama vile Naibu wa Spika amesema, tulinunua gari la maji lakini watu wa Igwamiti wananiuliza, ni kwa nini siwaletei ili ichimbe kisima cha maji? Wanauliza kwani hujaiona? Inaenda wadi moja au mbili? Hata sisi tunahitaji kwa sababu tulichaguliwa na Wanjiku kama hao wanaochimbuliwa maji. Ningetaka kusema ya kwamba tushikane pamoja.

Wakati nilikuwa hapa wiki jana, nilisema ya kwamba tutakaposhikana kama Wajumbe ishirini na watano, tutatoboa mlima wa Mt. Kenya tukiweza kuleta watu wawili pekee ili tupate kuwafundisha. Kitu cha pili, Naibu wa Spika, umwambie Gavana ya kwamba tunataka kukutana na yeye kwa sababu hatukuletewa wafanyikazi bali tuliletewa wanasiasa. Kama kwangu, huyo CO wa Barabara, kazi yake akileta taa moja, anaanza kutafuta kazi ya Mjumbe.

Wachira Karani alipewa kiti na watu wa Magharibi mwa Laikipia. Sasa unashindwa, ataangalia siasa au ataangalia vile watu wanagongwa huko. Ukienda ile njia ya K.C.C, kila wakati unakuta hadi wengine wameng'olewa meno na wengine wametendwa mambo mabaya kwa sababu hakuna mataa. Ni siku gani atatafuta mataa na pia afanye siasa?

Nyumba za Kaunti ndiye anapatiana hadi ukitaka kulipia ploti bado ni yeye. Sisi hatukuleta wanasiasa wengine juu yetu. Sisi ndio vigogo wa siasa lakini wale ni wafanyikazi wetu na sisi ndio tumewaajiri. Sasa leo tukiondolewa hiyo bajeti yote, wataenda wapi? Kwa hivyo Naibu wa Spika, uko na kibarua kigumu cha kuambia Gavana ya kwamba ni mimi ambaye nimeleta huo mjadala.

Mimi nililetwa hapa na watu wa Igwamiti na kama sio hao, singeingia katika hili Bunge. Wakati uliopita niliingia hapa nikiwa nimeteuliwa na wakati nimepata nafasi ya kuhudumia Wanjiku, mwingine hataki. Huwezi nivuta mikono au miguu wakati ninafanyia Wanjiku kazi. Kama sio hivyo, watu waonane ana kwa ana. Kwa hivyo Naibu wa Spika, uende utafute Gavana na usitetemeke anapofika huko. Ongea yale mambo kama vile naongea hapa. Ikiwa mimi natoa taarifa kwa nchi nzima, ni yeye tu nitakayeogopa? Mimi nitaongea kile ambacho kinanisumbua.

Kile ambacho kinanisumbua ni ya kwamba kila Mjumbe aliyechaguliwa yuko na shida kwake kwa sababu tunatandikwa usiku na mchana ya kwamba hatufanyi kazi. Sisi tumefungwa kwa sababu hatuna bajeti. Bajeti ikija inapelekwa *Executive* na sisi tunaanza kugawiwa chakula kidogo, haitawezekana. Mimi ukisikia nikisema ya kwamba haitawezekana, kila wiki nitakuwa nikitoa taarifa kwa wanahabari. Hiyo ofisi ni mimi nilijenga. Walipata kama nimejenga manispaa.

Ninashukuru Wajumbe wote na Spika kwa sababu mlisimama na Igwamiti na kuipitisha kufanyika manispaa. Wakati itatangazwa, tafadhali mje na msimame na watu wa Igwamiti na hiyo siku Bwana Spika uangalie hawa watu ishirini na moja. Kama Wachuka pekee singeweza kupitisha huo mswada lakini ni hawa Wajumbe Wangwana ishirini na moja ambao walipitisha. Kwa hayo mengi na machache, nasema ya kwamba ni lazima tuletewe watu wawili ili tupate kuwatengeneza na kuwapa dawa hadi washike laini. Tukishikiwa watu wawili, kutakuwa na laini.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor*

Speaker: Thank you, so much Hon. Wachuka, Members, I believe that you know that sneezing has no other particular name when it is being demonstrated. I want to give the chance to Hon. Salim, Member from Segera:

Hon. Salim Edung: Bwana Spika, nashukuru kwa kunipatia hii nafasi. Kitu cha kwanza ni pongezi kwa Mheshimiwa Umija kwa kuleta huu mswada katika hili Bunge. Yeye alijua ya kwamba yale mambo ambayo yanaendelea katika dunia nzima, kuna mambo mengi kuhusu mvua ambayo imeadhiri kila upande.

Bwana Spika, sijui kama umesoma kuhusu Mafarisayo katika Biblia? Sisi tulikuwa tunadhania ya kwamba wale watu ambao tulipatia kazi ni watu wangwana lakini kumbe kati yao kuna Mafarisayo. Ninaunga Mheshimiwa Wachuka mkono Pamoja na Naibu wa Spika ya kwamba yale ambayo wameongea hapa ni ukweli mtupu.

Ninaunga huu mswada 100% kwa sababu sisi tumeadhirika huko mashinani. Ukienda kila mahali, kuna shida ya Barabara na kuna watu ambao hawaishi kwao kwa sababu ya mvua. Ukienda sehemu za Naibor, kuna mahali kunaitwa Ranch mahali kuna daktari anayehudumu Lekiji. Nyumba yake ilipeperushwa na upepo na mabati zote zikatolewa hadi stakabadhi zake za kazi ziliharibiwa na sasa hivi anaishi kwa Jirani.

Nilienda nikapata Naibu wa Gavana na wale wengine na kuwalezea na kuwaambia ya kwamba kuna shida ambayo imetokea mahali na ningetaka wanisaidie. Jambo ambalo lilinikera na kunitia kiwewe katika moyo wangu ni kwamba waliniambia nipige picha, nilete makaratasi, chifu aandike barua ili huyo mtu apate kusaidika. Niliona ni kama ni kazi ya kuchunga kondoo au ng'ombe zake. Niliambia Naibu wa Gavana ya kwamba mimi siendi kufanya jambo kama hilo.

Huyu Naibu wa Gavana sio mara ya kwanza tumegongana naye. Hata siku ya siasa bado tuligongana naye na mpaka leo, ana huo uhasama. Mimi sitaogopa kumuelezea hata barabarani ya kwamba hataki kutusaidia. Ni vizuri kuambia mtu ukweli wa mambo kuliko kurudi nyuma. Ni afadhali kuambia mtu ya kwamba kama hataki kutusaidia, wakae na msaada wao.

Nikiangalia katika upande wa bajeti ambapo tunatenga pesa, tunataka kujua ni kiwango kipi cha pesa ambacho kilitumika mwaka uliopita na mwaka huu ndiposa tukitembea tunajua ya kwamba tumetumia pesa kiasi fulani. Mheshimiwa Wachuka amesema ya kwamba kuna vitu ambazo zilikuwa zinapelekwa huko. Mbona unapeleka hizo vitu na wewe mwenyewe unajipigia debe ya kwamba wewe ndio umenunua hizo vitu ilhali kuna pesa za Kaunti ambazo zimetumika kwa mambo ya dharura?

Tunahitaji kujua ni nani ambaye amesaidika kwa mambo ya dharura na ni pesa ngapi ambazo zimebaki. Bwana Spika, Pamoja na Naibu wa Spika, nyinyi ndio huwa mnaongoza hili Bunge na wakati jambo linatokea, ni lazima tushauriane kwa umoja ili tujue ni usaidizi upi tutapata. Nimeona Katibu wa Fedha katika hii Kaunti, ni kama jambo ambalo lilikuwa limetokea na Mackenzie ya kwamba msile chakula na msinywe maji ili mfe mwende Mbinguni.

Inaonyesha ya kwamba kuna fedha zetu ambazo tunadai, kuna watu ambao wanasema ya kwamba watatufanyia miradi lakini hakuna miradi ambayo inaonekana. Sisi tumeamua ya kwamba hapa hakuna mchezo sasa. Tunataka kujua yale ambayo inayofanyika hapa ili Wanjiku akiwa nyumbani aelewe kuhusu zile pesa za dharura na vile zinavyotumika. Ni siku chache zimebaki ili tuanze kufanya makadirio ya Bajeti kwa sababu mwaka unaisha. Hizo pesa, zimeenda wapi na ngapi ambazo zimebaki ili tujue mpangilio wa hizo pesa.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor*

Sisi katika hili Bunge hatuna mchezo kwa sababu Wanjiku ndiye alituleta hadi hapa. Kama kuna mtu alipewa kazi kwa kupitisha makaratasi yake katika hili Bunge na hafanyi kazi, nami pia naungana kwa sababu Mjeledi ni ule ule. Tuliahidiwa ya kwamba kutachimbuliwa visima mia tatu na Afisa Mkuu akaambiwa ya kwamba yeye ndiye atakayetengeneza ile kazi. Katika eneo langu, hakuna kisima hata kimoja ambacho kimetobolewa na Kaunti na zile ambazo ziko huko ni wafadhili kutoka Mbuga la Ol-pejeta, Segera, Impala na binadamu wenyeji.

Hao ndio wamenichimbia. Siwezi kusimama na kusema ya kwamba kuna kisima cha Kaunti ambacho kiko hapo. Mimi ningeomba ya kwamba ile mikakati yote na Barabara ambazo zimeharibika na ile pesa ambayo imetengwa ya dharura, ije ijenge hizo Barabara na wale ambao wako katika kambi wasaidiwe kama Wakenya wengine. Kama mtu binafsi anapeleka msaada kwa wale ambao wameadhiriwa, tunaulizwa maswali, je kwani msaada wa Kaunti uko wapi?

Chakula na vitu ambazo zinapeanwa sio za Naibu wa Gavana ilhali ni fedha za wananchi. Ni zile kodi ambazo zinarejea kwa wenyewe kununua hizo vitu. Kwa hayo machache, sisi tunaomba ya kwamba zile pesa za dharura zitumike vilivyo na Mungu wabariki. Asante.

Hon. Simon Kanyutu: Thank you, Mr. Speaker. I stand to support this motion by Hon. Umija about the victims of floods to be assisted through the emergency fund. Now, we are the ones who have been given the mandate to oversight the county and once we start crying, I wonder what our electorates will do. It is our obligation. If the issue we are speaking about in this Assembly persists, come 2027, we have our electorates and that is when we will realize that they are bitter. Not unless we act.

I remember in the previous regime in 2017, we had such an issue and all we are speaking here, we just need to have tangible evidence. If we are to bring any officer to enable us substantiate and ensure that whatever wrong has been done, we will have clear evidence because even that person has got a right to be defended and be heard on the issue.

On the issue pertaining to emergency fund, it is unless we make a policy. At the moment, we might ask for a statement on how the money has been utilized but because we do not have any policy guiding on how the money will be utilized, as we speak, maybe the money was utilized before the month of January. Therefore, it is good that we ask for a statement but without any power on how to manage the emergency fund, that is why you get an Honourable Member getting reports that other persons are claiming on their behalf because there is no policy.

Even if you have an issue following up on her, you might get her claiming that she used her own money but if she had utilized the emergency fund, she ought to have been open because the person in charge of that ward is the one who needs to oversight.

If everything is being done without his involvement, how will we be able to oversight without getting the information? Today this and this date, we have brought seven mattresses in your ward we have brought three spoons in your ward. It's unfortunate because we as Members elected and even those nominated, our work will be judged equally. No one will be a bit special unlike the others. On oversight, we will all be judged equally and whenever anything goes astray it is not one person who does it, it is all of us.

Not unless we join hands so that we will be able to follow up and see to it that whatever we pass here as an Assembly it is followed to the latter and it is done as per the budget that we

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor*

passed. Mr. Speaker, I support the motion by the Honourable Member. The Honourable from Segera talked of the challenges that he has encountered of trying to call the Deputy Governor and trying to trace his phone that is not being picked.

Phone picking doesn't bother me because you know, sometimes we make fun that this is a mobile phone. I might decide when you call, I am not ready to pick your call. If you could have an official code of communication, such that by the time we are seeking a statement, I will say I asked for assistance through this communication but they never got to may area yet we had an emergency.

I am sure following up is a bit itchy but Mr. Speaker, whatever we witness I will be able to join them we work together. If we have proper evidence, I will really support but if we just talk on what we have seen without concrete evidence, that one I cannot be part and parcel of. Mr. Speaker, I wish we follow our work to the end for this County to prosper. I am happy because I have heard many people claiming how they have got very nice promises. It is not only in their area but also even in my area I have heard of the same.

Mr. Speaker, what I do, I have been in politics for a duration and I know how to run away from it. If you promise people in my area, I just move away and claim you are the one who promised and not me. I stand firmly on that. If I make a promise or if we make a promise together, I tell my people it is until we pass the budget. That is when I will be very confident to promise them that we are doing this kind of work.

Without a budget, when I come to my people, I sweet-talk them and tell them it is better you hate me but I will tell you the truth. You will come to realise later that it is what is available and what that can be attained by our county funding. I support the Honourable Member's motion hoping the Emergency Kitty has not been exhausted. Thank you, Mr. Speaker.

Speaker: Thank you, Hon. Kanyutu. I now invite the mover of the motion to reply

Hon. Catherine Umija: Thank you, Mr. Speaker, I want to thank the House for contributing to this motion with such passion. I just want to remind the House that we are the Third Assembly and number three has a very significant importance especially if you are a person of spiritual beliefs. Number three, if you are a person that does not believe in Christianity or believe in other things, it is significant because when I look at the Greek philosophy, three is a number of harmony, wisdom and understanding.

When I go Biblically, the number three is a symbol of divine Perfection. I think this is the Third Assembly which is supposed to be representing those perfection, understanding and wisdom in whatever we do. I will quote the Bible as the Third Assembly, some of the Honourable Members have just said. If we do not take action, I will quote the bible, *"mene mene tekel upharsin."*

I think people will understand what I will say that we are going to be judged. Our days are numbered. If as a Third Assembly, we will look at things falling apart and we are all making noise and you are not taking action, we will be judged. The people will judge us as the Third Assembly. Let me tell you, the Executive will not be judged but the Assembly will be judged.

We have been given the responsibility by God Almighty to take care of our people. To take care of people who are suffering. People who have already encountered the floods victims, is not their fault, it's just a natural calamity but we have planned for it. We had put funds aside for it and we ensure that our people are actually given the services that they require.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor*

If we do not follow up, we will be judged and I repeat, *"mene mene tekel upharsin."* So, our elected Members and our nominated Members, let us take action and ensure that our people are served and that the County Executive is doing what they have been mandated to do. We as the overseers, we are there to oversee that every Shilling that has been set aside for the local citizen is actually sent to them. Thank you, Mr. Speaker.

(Question put and agreed to)

ADJOURNMENT

Speaker: The sittings of this House now stand adjourned until later today Tuesday, 21st May, 2024 at 2:30 p.m.

The House ended at 11.05 a.m.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor*